

WIZARA YA AFYA

MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA

USAJILI WA VYAKULA VILIVYOFUNGWA “PRE-PACKED FOOD”

UTANGULIZI

Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003 inamtaka kila anayejishughulisha na biashara ya vyakula nchini Tanzania, kusajili kwenye Mamlaka vyakula anavyovisindika au kuingiza nchini.

JE NI VYAKULA VYA AINA GANI HUSAJILIWA NA MAMLAKA?

Vyakula vinavyopaswa kusajiliwa ni vile ambavyo vimesindikwa na kufungashwa (Pre-packed food) kwenye makasha, kopo, chupa na kadhalika tayari kutolewa kwa mlaji moja kwa moja au kutumika kwa kupikia. Mfano wa vyakula hivyo ni nyama za makopo, vinywaji kama vile bia au soda na nyama za kwenye makopo. Maana hii haijumishi vyakula kama mahindi, maharage au karanga au vyakula ambavyo havijapitia hatua yeyote ya usindikaji.

UMUHIMU WA KUSAJILI VYAKULA

Vyakula vinasajiliwa kwa lengo la kuvifanyia tathmini ya usalama na ubora wake, pamoja na vifungashio vyake ikiwemo maelezo yaliyomo kwenye lebo ili kulinda afya za walaji wa vyakula kutokana na madhara yanayoweza kusababishwa kwa kula vyakula visivyofaa. Usajili husaidia kuzuia kutengeneza au kuingiza nchini vyakula ambavyo havijafikia viwango vya ubora na usalama.

UTARATIBU WA KUFUATWA WAKATI WA KUOMBA USAJILI

Mtu yeyote anayetaka kuagiza chakula kutoka nje ya nchi au kusindika chakula hapa nchini kilichofungwa kwenye makasha anapaswa kufuata taratibu na kanuni zifuatazo:-

1. Kujaza fomu ya kuomba usajili wa vyakula. Fomu ambayo hupatikana katika Ofisi za Mamlaka ya Chakula na Dawa na kwenye tovuti ya TFDA ww.tfda.or.tz
2. Kuwasilisha fomu hiyo kwa **Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), S.L.P. 77150, Dar es Salaam.**
3. Fomu hiyo iambatane na vitu vifuatavyo:
 - (a) Maelezo juu ya hatua za usindikaji wa chakula husika, mchanganyo wake, usalama wake na ubora wa

vifungashio vyake, na taarifa nyingine kama inavyoelekezwa katika Mwongozo wa Usajili wa Vyakula.

- (b) Sampuli za kutosha kwa ajili ya kutathmini maelezo ya lebo na uchunguzi wa Kimaabara wa chakula husika.
- (c) Ada ya Usajili.

MAMBO YANAYOANGALIWA WAKATI WA KUTATHMINI BIDHAA NA MAELEZO YA LEBO

Baada ya kupokea ombi la usajili wa vyakula, wataalam wa TFDA hutathmini maelezo kwenye nyaraka zote zilizowasilishwa. Sampuli hufanyiwa uchunguzi wa Kimaabara kwa lengo la kuona kama vyakula hivyo vina ubora na usalama unaokubalika na kuwa vifaa kwa matumizi ya binadamu. Tathmini huchukua muda mrefu kwa vyakula vyenye michanganyiko mingi. Wakati mwingine mawasiliano hufanyika kati ya Mamlaka na mwombaji ilikuthibitisha au kupata taarifa za ziada.

Tathmini ya maelezo ya kwenye lebo hujumuisha kuangalia maelezo kama yanajitosheleza kumfahamisha mlaji juu ya chakula husika na kama hayapotoshi. Pia lebo inabidi kuwa na maelezo kuhusu viambato na vikolezo vilivyomo, tarehe ya utengenezaji na maelezo ya mwisho ya matumizi, jina na anuani ya mtengenezaji. Maelezo haya inabidi kuwa katika lugha ya Kiswahili, Kiingereza au zote.

MAMBO YANAYOSABABISHA MAOMBI KUKATALIWA

Ombi la usajili hukataliwa pale tathmini ya taarifa na uchunguzi wa Maabara unapoonyesha kuwa chakula husika hakifai kwa matumizi ya binadamu au maelezo ya kwenye lebo yamelenga kupotosha na kumdanganya mlaji. Pia ikibainika kuwa bidhaa zimesindikwa katika jengo lisilokidhi mahitaji ya ubora na usalama.

IKIWA OMBI LA USAJILI LIMEKUBALIWA NINI KINAFUATA

Ikiwa ombi limekubaliwa mwombaji hupewa kibali cha kutengeneza chakula husika au kuingiza chakula hicho nchini. Kibali hudumu kwa muda wa miaka mitano na baada ya muda huo mwombaji analazimika kuleta upya maombi ya usajili.

MAMBO YA KUZINGATIA IKIWA UTAFAANYA MABADILIKO KWENYE BIDHAA YAKO

- (a) Endapo mwombaji atafanya mabadiliko kwenye mchanganyiko, vifungashio, maelezo kwenye lebo ya chakula husika anapaswa kutoa taarifa katika Mamlaka ili aweze kuruhusiwa kufanya mabadiliko hayo na Mamlaka iweze kuweka kumbukumbu zilizo sahihi.

- (b) Mwombaji anapaswa kuleta vielelezo na sampuli za bidhaa itakayobadilishwa.
- (c) Ikiwa mabadiliko yatahusu sehemu ya kusindika chakula husika mwombaji ataambatanisha pia ada ya ukaguzi wa jengo.

Chakula kikishasajiliwa ubora na usalama wake huendelea kufuatiliwa katika soko ili kuhakikisha kuwa kinaendelea kuwa na ubora uleule kama wakati wa usajili.

WITO KUTOKA MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA

Mamlaka inatoa wito kwa jamii yote ya kitanzania kushirikiana na Mamlaka katika jukumu la kulinda afya za walaji kwa kutoa taarifa pale wanapohisi kuuziwa chakula kibovu au pale sheria inapovunjwa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa anuani ifuatayo:

Mkurugenzi Mkuu

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA)

S.L.P. 77150

Dar es Salaam

Simu: 255 – 22 2450512/2450751/2452108

Fax: 255 – 22 2450793

E-mail: [tfda @ simbanet.net](mailto:tfda@simbanet.net)

Tovuti: www.tfda.or.tz